Kivu ya Kaskazini

Eti ndiyo mwisho wa vita vya ukabila ?

Kumefanyika manmotarehe 25 hadi 29 novembre, mkutano mkuu uliowakusanyisha pa Mwesso (ZTM) wajumbe wa makabila zilizo kuwa ndani ya fujo na vita mkali katika mitaa ya Walikale, Masisi na Rutshuru (bwito) tangu tarehe 20 march hadi mwezi wa nane mwaka huu pamoja na viongozi wa makanisa, wa mashirika yenyi kushurulikia maendeleo na wa sultani mbalimbali wa mikoa na vijiji vya mitaa hiyo.

Ukomo wa mkutano huo ulikuwa wa kuchungua na kujifunza kwa upeke visa vya vita hivyo vilivyo sababisha uaji wa watu kiasi cha elfu sita na wakimbizi zaidi ya elfu 200.

Katika mkutano huo wasimamizi wa kabila za wa Hutu, wa Tutsi, wa Hunde, wa Nyanga na wa Nande waliweza bila uoga kutoa maonyi yao yenyi kuelekea mwanzo na sababu za vita hiyo. Walitoa pia pendekezo (suggestions) na mahitaji yao kusudi katika siku za usoni kusukuweko tena mauaji ya namna hiyo. Wote pamoja walikubaliana kuwa sababu kubwa za fujo hizo ni kutoheshimishwa kwa sheria ya uraia, wivu, fujo kuhusu udongo na mahali ya kulima ao kufuga, uwongo, uyanguyangu, rushwa, kutokuwahazibu watu wakorofi, mafundisho mabaya ya mashirika ya ukabila (mutuelle ou ONG tribales), kabila moja kuwa tajiri ao kuwa na udongo wote kuliko lingine... Ingawa walikubaliana kuwa jambo lenyi kuelekea uraïa (nationalité) ao mikoa ya asili (collectivité-chefferie) ya elekea serkali kuu ya mji Kinshasa. Walioshiriki kunako mkutano wa Mwesso, Waliona kuwa makabila yote yenyi kwishi katika mitaa hiyo yapashwa kuwa na wasimamizi katika vituo ya uongozi, ila mble ya hayo serkali imeombwa ikamilishe hali binafsi ya kisheria (statut personnel ou juridique) ya kila mkaaji wa mitaa hiyo. Walikubaliana pia kuwa komiti zote za amani zilizoundwa kiisha vita zikubaliwe na liwali wa jimbo mbele ya kutumika. Kuhusu mikutano ya ukabila, imeombwa serkali iwe na muakilishi wake wakati kabila fulani ya kutana.

Mkutano wa Mwesso, ulisihi viongozi wa jimbo wachukue mipango ya kuwarudisha makwao wakimbizi na wakuu wao na kushurulika na ukingo wao wakati wanaporudi. Walihitaji kwa upande mwengine wale wote walioshiriki ao kuwasha moto ndani ya mauaji hayo kutiwa katika madaraka ya sherie na kuhazibiwa vikali kwa makosa walioyatenda.

Kabla ya kufikilia mapatano hayo, kila kabila lilitoa maonyi yake ya upekee kama vile wa Hutu na wa Tutsi walipendekeza zaidi kuigeuza mkoa wa asili "collectivité-chefferie" kuwa "collectivitié-secteur" ao tena kila sheria ya nchi iheshimu haki ya binadamu ao mara tena viongozi wote wa vijiji, mikoa wawe watu wenyi elimu.

Wa Hunde na wa Nyanga wamehitaji eti serkali ishurulikie uraia wa wananchi, wakikataa kugeuzwa kwa "collectivité-chefferie", wamesisitiza sana viongozi wa asili waliokimbia ao kuondoshwa, warudishwe kwa haraka madarakani ao tena kuomba serkali iheshimu na iheshimishe sheria alizozitia.

Kwa upande wao wa Nande, walionya serkali ichugue kwa makini tena kwa haraka hali ya uraia ya wa Hutu na wa Tutsi. Waliomba walinda amani wa kabila ya wa Hunde, wa Nyanga ao wa Hutu-Tutsi waondoshwe katika mitaa ya Rutshuru, Masisi na Walikale ao tena kuwanyanganya waaskari na wasiokuwa waaskari silaha wanazo kuwa nazo katika vijiji hivyo vya vita.

Mwishoe walionyesha matumaini yao ya kuona mikutano ya thawabu ya amani kama hiyo yafanyika katika mikoa mengine ya mitaa hiyo ya tatu na hata kunako daraja ya jimbo kusudi ya kukomesha fujo na mauwaji katika jimbo la Kivu.

Gabriël Lukeka bin Mlya

JE, UMESIKIA ...

Kwamba,
Ziwa ndogo lachipuka huko Muhumba mbele ya makao ya misionari moja mgeni ? Hata hivyo, majirani hushanga kuona namna gani ziwa hilo latukia wakati lingefutwa mahali pale. Na hiyo kwa kuacha njia ya maji mahali huyo misionari alipofunga. Ikingojewa jawabu, wapita-njia pamoja na magari wachafuliwa na kuogelea matopeni. Allah I Kweli, imeonekana kuwa chumba cha mazingira cha mji wa Bukavu na kile cha mtaa wa Ibanda vyafinyanga madaraka yao makubwa kwa kuokoa hali hiyo. Eti, hiyo ndio mtindo wa kisasa kwa kuonya maajabu ya mji kwa watalii.

Kuwa,
mwenyekiti wa mji wa Bukavu angepaswa kutoa machozi siku ile aliposikia eti muhuri wa chumba chake umepotea ? Uwizi ambao haukufanyiwa uchunguzi na wasemekana labda kaendeshwa na watu wanaoshiriki zaidi chumba hicho kinacholindwa usiku na mchana na askari jeshi wa usalama. Watu walingoja ya kuwa tangazo lililotolewa kwa jambo lile lipige marufuku vikartasi vyovyote vitakavyoonekana na muhuri ule baada ya kupotea kwake. He I hata leo hakuna lolote kafanyika, na mwezi pekee hana pupa ya kuuridisha wakati mahakama haijamnasa.

Eti,
mbali huko Punia jimboni mwa Maniema, kibarua katufikia cha kusema eti, kiongozi wa mtaa moja kazozana na mtumishi wake moja aliye mkuu wa mahali ahusikaye na usafirichaji. Kisa cha magongano : kutoa "Permis de conduire" ambayo mkuu huyo atoa baada ya kulipa feza nyingi sana. Kwa kukataa kwake, tume moja la hukumu katumwa kwa kuadibisha mtumishi ule. Yalioyotokea, ni kuharibika kwa kazi ile, ambako twashauri wakuu wa serkali mahali wajiongoze inavyostahili, siyo kama watu watokao juu wakati wa jamhuri ya pili ambao watu wengi waliishi migongoni mwa wengine. Huruma I

Kivu ya Kusini

Viongozi serkalini wayeyushwa ubongo

Mara nyingi viongozi serkalini jimboni mwa Kivu ya Kusini walikutana na wafanyabiashara pia viongozi wa mabenki kwa kutatua tatizo la kupandishwa kwa bei ya bizaa na hali ya kiychumi yazorota jimboni siku nenda rudi tangu hapo kabadilishwa feza. Kati ya wafanyabiashara watezamiwa wenyeji wa mashirika na maduka makuu kama vile Kotecha, Datco, Olive, Habib, Kamola na wengineo wenyi kuendesha kazi zao kwenyi soko kuu la Kadutu. Ila liwali wa jimbo husita kuwagusa na kuwaazibu, kwani wasemavyo, ajua mwenyewe sababu.

Kwa kweli, imeonekana kuwa wafanyabiashara huficha bizaa vyao na baadaye hupandisha bei ginsi wapendavyo na hakuna hata mkuu mmoja atiae kidole juu kwa kupinga jambo hilo na kuliazibu.

Kutokana na kufyatuka kwa bei ya vyakula na vifaa kwa mwendo wa kunguru ama mshale na ambao wanedeshwa na wafanyabiashara bila uwasiwasi na wasijue hata pato wanalo raïa walio wanunuzi wengi siku hizi za magumu. Ni toka vitendo hivyo, wakaaji wengi mjini Bukavu kaona ni vema kujieleeza nchini jirani hasa Rwanda ambako huuza vifaa kwa bei rahisi mara tatu. Pia ukosefu wa noti ndogo ndogo umesababisha hali hiyo. kwani wasema kuwaa viongozi wa mabenki noti hizo zimetumwa kununua zahabu mitaani Walungu, Mwenga, Shabunda, Fizi na kulipa walimu

Kweli kisingizio mtupu kwa kuwa siku za mwizi ni arubaini, watumishi wa mabenki na wengineo wafanyabiashara huuzisha feza hizo ugenini na hata mjini kwa bei wajua wenyewe wakizibadili kwa noti kubwa.

Kulingana na hali hiyo, yasemekana kuwa wa "bwana kuu" toka Kinshasa, viongozi serkalini kama vile wengineo, walijiruhusu kutumóa noti ndogo nchini jirani kwa kuzibadili na kupata feza za kigeni ambazo zaombwa na wenyeji wa manyumba. Kitendo hicho kimewaangamiza wakaaji ambao kapiga yohe wasijue nani awaokoe ingawa ingawa wakati huo viongozi walia machozi ya mamba wakiwachekelea raïa. Na mashirika kazaa kama hayo tuliyoyataja hapo juu hupandisha bei wasichurulike na chochote na hata mkuu moja asihusike kuwatisha kwani wapo washiriki.

Je mfuko moja wa mhogo kauze zaïre mpya 500, wa mchele 700, wa ngano 800, chupa la primus 15, bei ya upangaji nyumba haramu toka mfuko wa zeluji (ciment) wenyi bei ya zaïre 300 na zaidi hadi madolari za kiamerikani ingawa mshahara mdogo kweli. Toka zaïre 16 mpya na kazalika.

Kuona kama Wanazaïre walio na feza wafukuzia kununua biashara makwao, Wana-Rwanda kapunguza samani ya feza zetu wakizibadili 1NZ kwa franka 3 ya Rwanda pahali pa 23 na zaidi.

Ni hapo wakaaji kashikwa na hasira na kufunga mipaka kusiwe mtu wa kupita. Kuona hivyo, liwali wa jimbo kachukua hatua ya kukamilisha kitendo hicho. Kwa leo, nenda kaulize mabadilisho huko yakuwa ngapi ?

André Bisimwa L-B. Tserou

Ujanja wa Daktari Kakisingi waleta uwoga

Bibi Shaburwa alifia nini ?

Sheria inapowekwa ni lazima iheshimiwe. Habari zinazoaminika zajulisha kama mambo hayaendeki vizuri kunako hospitali ama "Kliniki" (Clinique médicale) ya mji wa Bukavu inayoongozwa tangu siku kadhaa na daktari Kakisingi, mganga na pia msimamizi wake aliyefikishwa mahakamani kujibu mashtaka. Ni siku nyingi swala hilo lawakera wakaaji.

Habari kamili ni kuwa mganga huyo amefungwa na kufunguliwa kwa mda kunako mahakama ya mji wa Bukavu mnamo tarehe na wiki yakukeshea siku kuu ya Noeli iliyopita mwaka 1993.

Yasemekana kama daktari Kakisingi, akisikilizana na mchungaji wa dawa ama Pharmacien wa hospitali hiyo, pia na wengine wafanyakazi anatumia mda wa siku nyingi shindano zisizo halali. Ahatarisha maisha ya maelfu ya watu na kuwatia wagonjwa uwasiwasi mda wa miezi sita sasa. Kwa kuwa anawapiga bila huruma shindano hizo zinazoweza kuwaambukiza ugonjwa na viini haramu vya ukimwi (Sida).

Hatari mlangoni kweli. Lakini wakati huohuo watu wengine wamewahi kusema kama ni wafanyakazi wa roho mbaya na wivu ndio wanamchukia daktari kijana huyo mushtakiwa Kakisingi na kumchochea maneno mengi kwa nia yakumtoa kazini ambako yeye ni kiongozi.

Basi ikiwa ni fitina ao uwivu, ni vema kungojea neno la mwisho la wenyi kuhusika na sheria mahakamani ambao watachungua maneno hayo na kuyakamilisha ao kuyakanusha, kuchukua hatua kali hata kufikilia kuhukumu faini ao kwenda jela, na hivyo, wakiisha uliza wataalamu na wangaga wengine.

Habari ya kifo inaosisimua mji wa Bukavu ni hiyo ya kutolewa dunia kwa bibi Anastasia Shaburwa Cito mtumishi hapo zamani kunako ofisi ya liwali wa jimbo la Kivu ya Kusini. Baada ya kushiriki kwenyi sherehe ya ndoa kunako chuo cha masomo ya Ibanda mnamo tarehe 18 desemba 1993, huyu kachukuliwa mahali yasiokajulikana na warugaruga. Na baada ya utafuti mwili wa bibi Shaburwa kagunduliwa katika shamba ya mihogo ya mtaani Ibanda. Mwili huyo umezikwa tarehe 6 januari 1994 kunako shamba la wafu la Brasserie. Lakini, mpaka sasa kisa cha kumua bibi huyo hakijulikane.

Wajambazi wa "Essence" wameshambulia gari la Bralima

Siku ya inne tarehe 30 desemba 1993, vijana wamoja wa pale Essence, mtaani Ibanda katika mji wa Bukavu wamejimiminavpombe ya primus bila kutoa pesa na kufikilia kuvunja gari la shirika Bralima lililokua likizunguuka kwa kuuzisha pombe Primus na kinywaji cha soda.

Walipokasirika mda wa miezi zilizopita na beyi kali ya vinywaji, beyi iliyozidishwa mara tatu kwa mda wa wiki moja, vijana hao shujaa na warugaruga wametenda kitendo kilicholeta msangao mkuu mjini Bukavu kwa jumla.

Wamempiga fimbo dereva Shababiri Karhebwa aliyekua akiongoza gari. Kiisha wakajibebea kwa kinguvu na ukali wao sanduku 510 ya pombe na kuvunja gari hio hata kufikilia kubeba "batterie" yake kwa hasira. Nia yao yakulichoma gari la shirika Bralima halikufikilia kutendeka kwa sababu askari-jeshi na walinda amani wamefika kiisha mda mfupi lakini ilikua ni nyuma mno.

Kwa kuwa wajambazi na vijana kazaa waliokua na kiu ya ngamia walikua wamekwisha kujinyangulia chupa na vifaa vingine na kutumia pombe ya shirika Bralima manyumbani mwao.

Hakika, kitendo hicho cha uizi na unyanganyi kimelaumiwa na wanainchi wote wenyi kutafuta na kuitaji nchi yetu ishike njia ya udemokrasia. Lakini ni vema pia shirika Bralima libadilishe beyi ya biashara yake kwa kuruhusu watu kuendelea kuvinunua bila matatizo ao misukosuko.

Saisho

Itakumbukwa kama katika toleo la 450 la gazeti letu ilijulishwa kuwa Mwami Ntambuka Balekage ni mwami kwa jumla. Mtaa wa Idjwi ulikuwa na mwami moja hapo awali ila kwa sasa umekwisha gawanyika kufuatana na agizo la Babu wa bami hao wawili kwa sasa. Mwami Ntambuka ni mwami wa Idjwi "Sud" na Rubenga ni mwami wa Idjwi "Nord". Na huko Idjwi ni Banjiji na Nkola wanaosimika bami katika mikoa hiyo mbili. Na mrizi wa Rubenga ambae ni Mwanae Ntawenderundi tasimikwa kiasili mwezi wa pili 1994 kama ilivyo desturi ya Bami kusimikwa baada ya siku 120. Na huyo mrizi ndiye mshauri wa bami wote jimboni mwa Kivu ya Kusini. Natumaini kuwa gazeti JUA litasaisha msemwa ule.

Mimi Balegamire Lubambo
Avenue Président Mobutu
Ibanda/Bukavu